

Utangulizi

● Namna ya kutumia kitabu hiki cha nyongeza

Kitabu hiki ni cha kujifundishia Sehemu ya Nne ya lugha ya Kijerumani kwa Redio *Deutsch – warum nicht?* Kama zile sehemu tatu za kwanza, kimekusudiwa kuwa kitabu cha marudio, wala hakikusudiwa kuwa kitabu cha kujifunzia mwenyewe.

Kwa hivyo jaribu kila mara kusikiliza kwanza mafunzo yenyewe redioni kabla hujakifungua kitabu hiki.

Mazoezi ya kusikiliza kila somo redioni yatakusaidia kufahamu vyema zaidi yote yaliyo muhimu. Hii ni kumaanisha kuwa ufahamu kwa jumla yale yanayotokea, mifano inaonyeshwa wapi, nani anazungumza na nani, wahusika wanazungumza nini na wamo katika hali gani. Jaribu kuyashughulikia yote na kumbuka kuwa si lazima ufahamu neno kwa neno.

● Nini kipya katika Sehemu ya Nne?

Sehemu ya Nne inahusika na mikoa mitano ya Mashariki ya Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani – Brandenburg, Mecklenburg, Pomerania ya Magharibi, Saxony, Saxony-Anhalt na Thuringia – iliyokuwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Ujerumani (Ujerumani ya Mashariki) hapo awali. Mara nyingi sehemu hii huitwa mikoa “mipya” kwa sababu imejiunga na mikoa kumi na moja ya zamani ya Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani (Ujerumani ya Magharibi) wakati Ujerumani ilipounganishwa tena 1990. Habari za kimsingi kuhusu historia ndefu, utamaduni na jografia ya mikoa hii, hutolewa kama utangulizi. Masomo matano yanayojishughulisha na mikoa ya Mashariki ya Ujerumani, husimuliwa kama ripoti za redioni, msimulizi akiwa Andreas. Kila moja ya masomo hayo matano hufuatiliwa na masomo yanayoingilia mambo mbali mbali juu ya mkoa unaohusika, kama vile mandhari yake, viwanda, kazi za mikono na utamaduni. Masomo haya husimuliwa katika aina ya mazungumzo, hadithi na mashairi.

Wahusika muhimu katika Sehemu ya Nne ndio wale wale kutoka sehemu tatu za kwanza.

- **Andreas** ni yule aliyekuwa mwanafunzi ambaye wakati huo huo alikuwa akifanya kazi ya mpokezi katika Hotel Europa. Amekwisha maliza masomo yake na sasa anaripoti redioni juu ya mikoa hii mipya ya Shirikisho katika Mashariki ya Ujerumani.
- **Ex** ni kijizimwi jike kutoka mawazoni tu. Hawezi kuonekana kwa macho, lakini sauti yake inasikika vizuri.
- **Dr. Thürmann** amefunga afisi yake ya udaktari mjini Berlin na amerudi kwao Leipzig. Sasa anajishughulisha na uandishi wa makala juu ya elimu ya matumizi ya miti shamba.

- **Frau Berger** aliwahi kuwa meneja wa Hotel Europa mjini Aachen. Ameiua hoteli hiyo na angependa kununua hoteli nyingine Mashariki ya Ujerumani kwa sababu angependa kujaribu kitu kipya. Mara kwa mara hufuatana na Andreas katika safari zake za kikazi.
- **Hanna Clasen** ni msichana anayesafisha vyumba katika Hotel Europa. Karibuni ataolewa na anataka kuacha kazi.

Muundo wa masomo ni ule ule kama ulivyokuwa katika sehemu tatu zilizopita. Kwanza utasikia mazungumzo au ripoti, kisha maelezo yake. Baadaye yatafuatia maelezo ya sarufi, kisha hapo utaweza kuyasikia tena mazungumzo. Maandishi katika Sehemu ya Nne ni magumu kidogo yakilinganishwa na sehemu tatu za kwanza.

Mwanzoni mwa Sehemu ya Nne tutawajulisha tena wahusika muhimu, hasa wale wasikilizaji ambao hawakuwa na bahati ya kusikiliza sehemu tatu za kwanza.

● Yaliyomo katika Kitabu cha Nyongeza

A Habari kuhusu kila somo

1. Muhtasari wa sarufi

Humu mmetolewa muhtasari wa sarufi muhimu kutoka kila somo. Sarufi hiyo inaelezwa kwa ufafanuzi kwa kutolewa mifano kutoka kila somo. Katika masomo kadha sarufi hufuatiliwa na habari za kimsingi kuhusu mada inayozungumzwa.

2. Maandishi katika kila somo

Maandishi yanayotolewa katika aina ya ripoti za redioni, mazungumzo, maelezo, maswali na majibu au mashairi, yameandikwa kwa Kijerumani baada ya muhtasari wa sarufi. Ili kukuwezesha ufahamu kwa wepesi, maandishi hayo yametanguliwa na maelezo mafupi kwa Kiswahili. Kwa hivyo, ukikosa kusikiliza somo moja redioni, unaweza kulipitia tena somo hilo kitabuni.

3. Mazoezi

Sehemu kubwa ya mazoezi inaelezea sarufi, lakini yako pia mazoezi ya ufahamu (comprehension) wa maandishi na maneno, kwa mfano kujaza jadwali ya maneno pamoja na matumizi sahihi ya maneno na vifungu vya maneno. Katika mazoezi ya ufahamu, unatakiwa usikilize masomo na kuamua maandishi yapi kutoka mazoezi yanatoa habari sahihi. Panapohitajika, unaweza kutazama kwenye mazungumzo yaliyochapishwa kikamilifu katika kila somo. Majibu ya sehemu kubwa ya mazoezi utayakuta katika ufafanuzi wa mazoezi mwishoni mwa kitabu.

Ufafanuzi wa mazoezi unatoa majibu kwa mazoezi yale yenye uwezekano wa jibu moja tu sahihi. Penye mazoezi yasiyokuwa na uwezekano wa jibu moja sahihi, ufafanuzi wa mazoezi hutoa mifano ya kukuongoza. Pale unapotakiwa utumie uhuru wako mwenyewe wa kujibu, hakuna majibu katika ufafanuzi wa mazoezi.

B Muhtasari wa sarufi

Hapa pametolewa muhtasari wa sarufi mpya katika Sehemu ya Nne. Sarufi muhimu katika Sehemu ya Nne ni:

- Vitenzi visaidizi (subordinate clauses), maswali yasiyo ya moja kwa moja (indirect questions), vitenzi visaidizi vinavyotumia wakati (subordinate clauses of time) vinavyoanzia kwa *wenn*, vitenzi visaidizi vinavyoanzia kwa *um ... zu*, *obwohl* au *damit*, vitenzi vya mahusiano (relative clauses), sentensi zinazotumia shuruti (conditional sentences), vitenzi vyenye kutumia kitenzi-jina (infinitive), wakati wa kitendo chenye shuruti (conditional tense), hali ya kutazamia (-nge...-) katika wakati uliopita (imperfect subjunctive) wa *sein* na *haben* na wa vitendo vya utaratibu (modal verbs),
- Vitendo jirejee (reflexive verbs), vielezi viwakilishi (pronominal adverbs) *damit*, *davon*, *darüber*... mlinganisho wa vivumishi vya sifa (adjectives).

C Ufafanuzi wa mazoezi.

Ufafanuzi wa mazoezi unatumiwa kuhakikisha iwapo umetoa majibu sahihi kwa mazoezi kutoka kila somo.

D Tafsiri ya mazungumzo

Tafsiri ya mazungumzo imekusudiwa kukusaidia ufahamu kwa urahisi zaidi, hasa kama hukuweza kujiunga nasi katika sehemu tatu za kwanza na hujui maana ya maneno au sarufi iliyokwisha elezwa.

E Orodha ya maneno kwa mujibu wa alfabeti

Humu utayakuta maneno yote mapya yaliyotumiwa katika Sehemu ya Nne. Maneno yaliyotumiwa katika sehemu tatu za kwanza hayakuorodheshwa hapa. Namba iliyowekwa ndani ya mabano (brackets) hukukumbusha somo lilimotumiwa neno kwa mara ya kwanza.

Huenda umekwisha sikia kuwa mafunzo haya ya Kijerumani yanatangazwa kote duniani katika lugha nyingi mbali mbali. Kwa sababu hii tunasikitika kuwa hatuwezi kuzingatia mambo maalumu yanayohusika na utamaduni na lugha ya nchi yako. Hata hivyo, tunaamini kuwa wewe mwenyewe ndiye mtu bora kabisa wa kuweza kuamua juu ya tafauti na mlingano uliopo baina ya Kijerumani na lugha yako mwenyewe.

Ni matumaini yangu kuwa utayafurahia masomo haya na kwamba utafanikiwa na mafunzo haya yaitwayo *Deutsch – warum nicht?*

Herrad Meese